Kwanini biblia iwasifu wenye kutumia shoto zaidi ya wanaotumia kulia? *(Waamuzi 20:16).*

---

Swali: Je kuna jambo gani la ziada katika mkono wa kushoto hata watajwe kama mahodari katika vita?.

Jibu: Turejee…

> *Waamuzi 20:16 "Katika watu hao wote walikuwako watu waume mia saba waliochaguliwa, wenye shoto; kila mmoja alikuwa anaweza kuutupia unywele mawe kwa teo, wala asikose".*

Ni kweli zipo tafiti zinazoonyesha kuwa mkono wa kushoto una nguvu (uwezo) kuliko ule wa kuume (kulia).

Lakini hiyo si sababu biblia iliyoitumia kuusifiia mkono huo(wa kushoto) zaidi ya ule wa kulia…kwasababu pia walikuwepo mahodari waliotumia mikono yote miwili na walionekana sawa tu..

> *1Nyakati 12:2 "Walikuwa wenye kupinda upinde, nao walikuwa hodari wa kutumia mkono wa kuume na wa kushoto, kwa kutupa mawe ya teo, na kwa kupiga mishale ya upinde; walikuwa wa nduguze Sauli, wa Benyamini".*

Sasa ni sababu gani inayowafanya wanaotumia shoto kuonekana mashujaa zaidi?.

Jibu, Sababu kuu ni mbinu za upiganaji.

Kawaida ni kuwa idadi ya askari wanaotumia mkono wa kulia (kuume)…ni kubwa kuliko ile ya wanaotumoa shoto.

Sasa kikawaida inakuwa ni ngumu sana kupambana na mtu anayetumia mfumo mwingine tofauti na wa kwako, lakini mfumo unaofanana na wewe ni rahisi kumsoma, na kumwingia.

Ni rahisi sana mashoto kupambana na mashoto wenzake na kulia kupambana na kulia mwenzake..lakini inapotokea kinyume na hapo, basi vita vinakuwa vigumu kwasababu ni mifumo miwili tofauti.

Na kwasababu mashoto ni wachache na wengi wanaokutana nao wakati wa vita ni watu wanaotumia mkono wa kuume (kulia), basi wanapata mzoefu mkubwa wa kupambana na watu wa tofauti na mikono yao, na kuwafanya kuwa hodari zaidi..

Lakini wale wanaotumia kulia, wanakuwa na uhodari hafifu kwasababu ni mara chache sana wanakutana na wasiotumia mashoto, hiyo inawafanya uzoefu wa kupigana na jamii hiyo ya watu kuwa mdogo, na kuwafanya kuanguka (kupigwa) wanapokutana na watu wanaotumia mashoto, hiyo ndio sababu kuu…

Na sababu nyingine inayowafanya watu wanaotumia mashoto kuwa hodari zaidi katika biblia, ni uwezo wa kuficha jambo bila kujulikana..

Kikaiwaida askari anajulikana kwa kuhifadhi upanga wake upande wa paja lake la kushoto, lakini wale wanaotumia mashoto huficha panga zao upande wa kuume, jambo linalowafanya wasifahamike kwa haraka kama ni maaskari..

Jambo hilo tunaliona kwa Ehudi aliyekuwa mwamuzi wa Israeli.

*Waamuzi 3:14 “Wana wa Israeli walimtumikia Egloni mfalme wa Moabu muda wa miaka kumi na minane.*

*15 Lakini wana wa Israeli walipomlilia BWANA, BWANA akawainulia mwokozi, Ehudi, mwana wa Gera, Mbenyamini, mtu aliyekuwa mwenye shoto; nao wana wa Israeli walimpelekea Egloni mfalme wa Moabu tunu mkononi mwa huyo Ehudi.*

*16 Ehudi alijifanyia upanga uliokuwa na makali kuwili, urefu wake ulipata dhiraa moja; akaufunga huo upanga ndani ya nguo yake katika paja lake la MKONO WA KUUME…………*

*20 Basi Ehudi akamwendea; naye alikuwa anaketi peke yake katika chumba chake cha baridi. Ehudi akasema, Mimi nina ujumbe utokao kwa Mungu kwako wewe. Basi akainuka katika kiti chake.*

*21 Ehudi akaunyosha mkono wake wa kushoto, akaushika huo upanga kuutoa hapo katika paja lake la kuume, akamtia tumboni mwake;*

*22 hicho kipini nacho kikaingia ndani pamoja na huo upanga*

> *wenyewe; nayo mafuta yakashikamana tena juu ya upanga, kwani hakuutoa tena upanga tumboni; nao ukatokea kwa nyuma"*

Bwana atupe kutumia mashoto mbele ya adui wetu ibilisi, tupiganapo vita vya kiroho.

> *Waefeso 6:14 "Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani……..*
>
> *17 tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu"*

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP,

jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>
https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

LIPO LA KUJIFUNZA KWA WALE MASHUJAA 37 WA DAUDI.

Nini maana ya Dirii, Chapeo na Utayari?

Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu (Zekaria 13:7-9)

MAANA ROHO HUCHUNGUZA YOTE, HATA MAFUMBO YA MUNGU.

TUTAMPIGA KWA NDIMI ZETU.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp